



Msimlaani, Wallahi, namuapa Mwenyezi Mungu sikujua lolote kwake isipokuwa anampenda Mwenyezi Mungu na Mtume wake

Imepokelewa kutoka kwa Omari bin Khattwab -radhi za Allah ziwe juu yake-: Ya kwamba mtu mmoja alikuwa katika zama za Mtume rehema na amani ziwe juu yake jina lake anaitwa Abdallah, na alikuwa akitaniwa kwa jina la Punda, na alikuwa akimchekesha Mtume rehema na amani ziwe juu yake, na alikuwa Mtume rehema na amani ziwe juu yake amekwisha mchapa viboko kwa sababu ya ulevi, basi akaletwa siku moja akaamrisha akachapwa, akasema mtu mmoja katika jamaa waliopo: Ewe Mwenyezi Mungu mlaani, ni mara ngapi analetwa!? Akasema Mtume rehema na amani ziwe juu yake: "Msimlaani, Wallahi, namuapa Mwenyezi Mungu sikujua lolote kwake isipokuwa anampenda Mwenyezi Mungu na Mtume wake".

[Sahihi] [Imepokelewa na Al-Bukhaariy]

Katika zama za Mtume rehema na amani ziwe juu yake kulikuwa na bwana mmoja jina lake Abdallah, na akiitwa Punda, kwa jina la utani, na alikuwa akimchekesha sana Mtume rehema na amani ziwe juu yake katika baadhi ya maneno yake, na alikuwa Mtume rehema na amani ziwe juu yake amekwisha mchapa kwa sababu ya kunywa pombe, siku moja akaletwa tena akiwa amekunywa pombe, akaamrisha akachapwa. Mmoja kati ya waliopo akamtukana, na akasema: Mwenyezi Mungu mlaani, amezidi sana kuletwa kwa sababu ya kunywa pombe?! Akasema rehema na amani ziwe juu yake: Msimuombe kufukuzwa katika rehema ya Mwenyezi Mungu, na Wallahi sijajua lolote kwake isipokuwa anampenda Mwenyezi Mungu na Mtume.

<https://www.sunnah.global/hadeeth/sw/show/66214>

